Iran ya Kikhomeiny ni Dola ya wanamgambo sio dola ya utawala wa sheria

Kimetayarishwa na
Jopo la Wataalamu katika Dar Almuntaqaa

Kimetafsiriwa na
Omar Khalfan Ali
na
Juma Yussuf Khamis
Zanzibar

بسم الله الرحمن الرحيم

Shukrani zote zinamstahikia Allah (s.w) Mola wa viumbe wote, na sala na salamu ziwe kwa Mjumbe wake na jamaa zake na maswahaba zake na watakaomfuata.

Dola ya Kikhomeiny ya Iran tokea kuanza kwake pale Alkhomeiny alipofanikiwa kumpindua Shaah na kutwaa uongozi, inaendelea kufanya uadui na ugaidi dhidi ya majirani zake kwa kisingizio cha kutanua mapinduzi. Inafanya hivyo kwa akili za wana mgambo ambazo hazizingatii kanuni, sheria na hata mila, na hili sio geni kwa wale wanaojua itikadi inayobebwa na muasisi wa dola ya kimapinduzi ya Iran, au njia iliyotumika kuijenga dola hii na kukipa mamlaka kamili Kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi wa kutawala idara zote na wao kuwa juu ya sheria na kanuni. Na hapa tutaelezea kwa ufupi mawazo ya Alkhomeiny na walinzi wa Mapinduzi na jarima zao ambazo zinalifanya Dola hili liwe ni Dola la wanamgambo na sio Dola la utawala wa sheria.

AL KHOMEINY MUASISI:

Ruuhullah Almuusawy Alkhomeiny (1900 - 1989) ndie muasisi wa Dola ya Kikhomeiny mwaka 1979 ambayo iliendeshwa kwa mtindo wa dola ya Swafawiyya ambayo ilifuata nadharia ya utawala wa Faqihi wa ujumla usio mipaka ambao ulimfanya yeye awe ni Imam wa kumi na tatu (13) wa Shia wa Ithnaasheria.

Yameandikwa mengi kuhusu mtu huyu na yale mambo yaliyo saidia kufanikiwa kwa Mapinduzi yake kwa kuungana kwake na nchi za magharibi, lakini kwa sasa hatuzungumzii hilo.

Kwanza: Itikadi ya al KhomeinY

Alkhomeiny amekusanya shudhudhi za Itikadi ya kishia pamoja na falsafa potofu ambayo aliisoma na kuisomesha, jambo ambalo limemzalishia fikra kali zinazolenga kwenye mapambano na mapigano. Alkhomeiny alikua yuko mstari wa mbele katika majamaati ya kishia, pamoja na kwamba hakua na elimu na fiqhi ya maeneo hayo. Hotuba zake kali zilikua na athari kubwa kwa wasikilizaji wake, na hapo alipata fursa nzuri ya kueneza shudhudhi zake za kifikra na kiitikadi.

Na sisi tutataja hapa zile itikadi zake mashuhuri ambazo zinakwenda kinyume na Qur-ani na Sunna:

1. Alkhomeiny anasema: Sisi hatumuabudu Mungu ambae anajenga jengo kubwa la uungu na uadilifu na dini kisha analiharibu kwa mikono yake.

(Sisi tuna muabudu Mungu ambae tunajua kwamba matendo yake yana zingatia msingi wa akili wala hafanyi matendo yanayo kwenda kinyume na akili, na sio Mungu ambae anajenga jengo kubwa la uungu na uadilifu na dini kisha analiharibu kwa mikono yake, na anampa uongozi Yaziid na Muawiyya na Othman na mfano wao miongoni mwa muhajirin, wala

haelezei kinacho takiwa kwa watu milele baada ya Mtume (saw), ili asipate kusaidia katika kujenga jengo la dhulma na kudhulumiana), (Kashful asraar, 116 - 117).

2. Alkhomeiny anakubali Uwepo wa kubadilishwa kwa Qur ani tukufu :

(...na hii ni moja ya maana ya tahriif (kubadilishwa) ambako kumejitokeza katika vitabu vyote vya Mbinguni ikiwemo na Qur-an tukufu na aya zake, vyote vimewekwa katika mikono ya waja baada ya mabadiliko mbalimbali kwa mujibu wa uteremkaji wake na hatua zilizo pitia, tokea mwanzo hadi mwisho).

Na idadi ya hatua za tahriif zinaendana na idadi ya siri za Qur-ani, zinafanana kama vinavo fanana viatu. [kitabu cha Al qur-ani : babu maarifatullah, 50].

3. Alkhomeiny anafanya ilhadi katika aya za Allah na anatafsiri kauli ya Allah isemayo :

﴿يُدَبِّرُ ٱلْأَمْرَ يُفَصِّلُ ٱلْآيَٰتِ لَعَلَّكُم بِلِقَآءِ رَبِّكُمْ تُوقِنُونَ﴾ kasema "**ربكم**" **yaani Imamu ?!** (Raad/2), kasema: Yaani rabbukum ambae ni Imamu, angalia namna gani yalivo pangika maneno ya Allah na vilivyo umbika viumbe wake [misbahu lhidaya ilaa lkhilafati walwilaya, 150].

4. Alkhomeiny anasema: Mtume (saw) hakupata tawfiiq katika daawa yake!!??

(Kadhia ya kufichikana kwa Imamu ndio kadhia muhimu inayo tubainishia mambo mbali mbali, katika hayo ni kwamba haiwezekani kwa mtu yeyote kutimiza amali kubwa kama hii ya kujenga uadilifu uliokamilika ulimwenguni kote na kwa watu wote, isipokuwa Mahdy Almuntadhar (sa) ambaye Allah Mtukufu amemueka akiba kwa ajili ya viumbe. Kila Mtume alikuja kwa lengo la kusimamisha uadilifu, na lengo lake lilikuwa kwa ulimwengu mzimza lakini hakupata mafanikio. Na hata Mtume wa mwisho Muhammad (saw) na yeye pia alikuja kwa ajili ya kuwatengeneza watu na kuwapamba vizuri na kutekeleza uadilifu lakini na yeye pia hakufanikiwa, na kwamba atakae fanikiwa kikamilifu na kutimiza uadilifu katika pembe zote za ulimwengu ni Mahdy peke yake), [Mukhtaratun min ahadiith wa khitwabatul Imamul Khomeiny, 2/43].

5. Alkhomeiny anamtuhumu Mtume kwa kuogopa kufikisha amri ya Allah kwa khofu ya kuja kubadilishwa Qur-ani:

(kwa mkusanyiko wa dalili hizi na mapokezi ya hadithi inatubainikia kwamba Mtume alikua anaogopa kulingania Uimamu, na atakae rejea katika vitabu vya tarekhe na historia atajua kuwa Mtume (saw) alikua na haki ya kuogopa, lakini Allah akamuamrisha afikishe na akamuahidi kumlinda), [Kashful asrar, 150].

(Tumethibitisha mwanzo wa mazungumzo haya kwamba Mtume alijizuilia kuzungumzia uimam katika Qur-ani kwa kuogopa kuwa Qur-ani isije ikakumbwa na tahriif baadae), [Kashful asrar, 149].

6. Alkhomeiny anamtuhumu Mtume kwa kushindwa kufikisha ujumbe:

(Ni wazi kwamba Mtume kama angefikisha ujumbe wa uimamu kama alivyo amrishwa na Allah na akafanya jitihada katika jambo hilo kusingetokea tofauti, mapigano na vita baina ya nchi za Kiislamu na kusingelikuwa na tofauti katika misingi ya dini na furui zake (matawi yake)), [Kahful asrar,155].

(Kwa hakika Manabii wote walikuja kwa lengo la kuweka misingi ya uadilifu ulimwenguni lakini hawakufanikiwa, hata Mtume Muhammad (saw) ambae ni Mtume wa mwisho katika Mitume nae pia alikuja kuwatengeneza waja na kutandika uadilifu pia na yeye hakufanikiwa katika hilo), [Kitabu Nahjil Khomeiny, 146].

7. Alkhomeiny anasema: Mtume (saw) hakuweza kuipata serikali aitakayo!!!

(Ninasikitishwa na mambo mawili, moja lina sikitisha zaidi kuliko jengine. La kwanza ni kwamba tokea mwanzo wa uislam na utume na zama zilizofuata, hawakuachia kudhihiri serikali inayotakiwa na uislam. Katika zama za Mtume (saw) kwa sababu ya matatizo mbalimbali ya kivita na upinzani haikupatikana serikali kama alivyoitaka Mtume (saw). [Mukhtaraatil ahaadiith wakhitaabatil Imam Alkhomeiny, 2/520].

8. Alkhomeiny anathibitisha uwepo wa Mtume mwengine anaepokea wahyi, na miongoni mwa wahyi huo ni kuhusu Mapinduzi yake :

(Fatma Zahraa baada ya kufa kwa baba yake alikuwa na huzuni kubwa siku 75, na Jibril alikuwa anamjia kumliwaza na kumjulisha mambo ambayo yatatokea siku za mbele. Na niwazi kwa mujibu wa riwaya hii kwamba Jibril katika kipindi hicho cha siku 75 alikuwa anakuja mara kwa mara kwa Fatma, wala sidhani kuwa riwaya mfano wa hii imewahi kutokea kwa mtu yeyote ukiacha mbali wale Manabii wakubwa, na Imam Aliy alikua anaandika mambo haya aliyokua analetewa Fatma na Jibril!, na inawezekana kwamba kadhia za Iran ni katika jumla ya mambo aliyoletewa).

(Khutba ya Alkhomeiny kwa mnasaba wa siku ya mwanamke huko Iran tarehe 2/3/1986 na imetangazwa na redio Tehran kwa sauti yake na kunakiliwa na magezeti mbalimbali ya kiarabu).

9. Alkhomeiny anathibitisha msahafu mpya mbali na Qur-ani Tukufu:

(Hakika Jibril alikuwa anakuja kwa Bi Fatma baada ya Mtume (saw) kumletea khabari za ghaib!! na Amiirul Muuminiin akawa anaziandika, na huu ndio Mus-haf Fatma), [kashful asrar, 143].

10. Alkhomeiny anadai kwamba Aliy ndie msimamizi wa kila nafsi na inacho kichuma:

(Hakika yeye alayhi salam ndie mwenye utawala usio mipaka... kwani yeye alayhi salam kwa utawala wake waujumla huisimamia kila nafsi na ilicho kichuma kwa ujumla, na kila kitu kiko pamoja na usimamizi wa kivuli cha uungu), [Misbaahul hidaya ilal khilalaafati wal wilaya, uk155].

11. Alkhomeiny anasema: Aliy angedhihiri kabla ya Mtume angeidhihirisha sharia na angekua Mtume!!

(Kama Aliy (as) angedhihiri kabla ya Mtume angelidhihirisha sharia kama alivyoidhihirisha Mtume (saw) na angekuwa Nabii aliye tumwa kwa watu, kwa jinsi walivyoungana kiroho na darja zinazo onekana na zisizo onekana, [Misbaahul hidaya ilal khilalaafati wal wilaya, uk153].

12. Alkhomeiny anasema: Aliy ni kila kitu kwetu na anachukua nafasi ya mwanzo katika mambo yetu yote ya kiutu na wajibu wetu ni kumfuata!!

(Ni lazima mambo yenu yote yafuate riadha na malezi ya kiroho. Muangalieni Aliy (as) popote tunapo kwenda tunaliona jina lake! Kwa wanafiqhi tuna sikia kuhusu fiqhi ya Aliy (as), na kwa watu wa zuhdi tunasikia kuhusu zuhdi ya Aliy (as), na kwa watu wa tasawwuf tunasikia

kuhusu tasawwuf yake (as), na tunapokwenda kwa watu wa riadha ya kiroho tunawaona wana kariri jina la Aliy (as) na wanaanza riadha yao kwa kutaja jina lake. Aliy huyu ndiye kila kitu kwetu, yeye anachukua nafasi ya mwanzo katika mambo yetu yote ya kiutu, na wajibu wetu sote ni kumfuata. Katika ibada ilikuwa ibada yake iko juu zaidi kuliko ibada za wengine, na katika zuhdi alikua anawashinda watu wote wa zuhdi, na katika viwanja vya vita alikua anawashinda wapiganaji wote, na kwa upande wa nguvu alikua anawashinda wenye nguvu wote, alikua ni mtu wa ajabu alie kusanya sifa tofauti), [Mukhtaraatil ahaadiith wa khitaabaatil Imamul Khomeiny, 1/294]

13. Alkhomeiny anaitakidi kuwa maimamu wana sifa ya kujua kila kitu na kukisimamia:

(Manabii na mawasii (as) wanadaraja kubwa za kiroho zinaitwa roho takatifu na kwa kupitia hali hiyo wana uwezo wa kujua na kusimamia viumbe wote mpaka chembe ndogondogo kabisa), [Al arbaun hadithan, Alkhomeiny, 597].

14. Alkhomeiny anasema: Hakuna anaeweza kufikia katika darja ya Maimamu, si Malaika alie karibu wala Mtume mwenye kutumwa!

(Katika mambo muhimu ndani ya madhehebu yetu ni kwamba hakuna anaefikia darja za Maimamu hata Malaika waliokaribu na Mtume mwenye kutumwa), [Al hukumal Islaamiyya, 93].

15. Alkhomeiny anasema: Maimamu wanahudhuria katika vichwa vya watu wanaoelekea kufa!

(Kama tunavyo itakidi sisi na wao wanaitakidi hivyo hivyo na khabari mbalimbali zinazungumza kwamba Amirul Muuminiin (as) anahudhuria katika vichwa vya wanaotaka kufa ikiwa ni muislamu au kafir au mnafiki), [Al maad fi nadharil Imam Alkhomeiny, uk 177].

16. Alkhomeiny anasema: Vitabu vya amali vina pelekwa kwa Mahdi wa Shia.

(Tuna uwezo wa kuangalia hali ya vitabu vya amali zetu kabla hazijapelekwa kwa Mola Mtukufu na kabla havija pelekwa kwa swahibu zamaan (sa), kwani vitabu vya amali zetu hupelekwa kwa Imam swahibu zamaan (sa) mara mbili kwa wiki kwa mujibu wa riwaya), [Almaad fi nadharil Imam Alkhomeiny, 368].

17. Alkhomeiny anaona mazazi ya Mahdi ni makubwa zaidi kuliko mazazi ya Mtume (saw)!

(Hakika mazazi ya Imam Mahdi ni sikukuu kubwa kwa waislamu!? na inasadikika kwamba ni kubwa zaidi kuliko mazazi ya Mtume Muhammad), [Wasiyyatul Khomeiny, uk 47].

18. Alkhomeiny anamkufurisha Abuu bakar na Omar na anawapa sifa za ujinga, upumbavu, uzushi na uzandiki!!

(Sisi hapa hatuna khabari na mashekhe wawili na yale waliyoyafanya ya kuipinga Qur-an, na kuzichezea hukmu za Mungu, na walichojihalalishia na kujiharamishia wenyewe, na udhalimu walioufanya... lakini sisi tunaashiria kutojua kwao hukmu za Mungu na dini. Na mfano wa watu hao majahili, wapumbavu, wazushi, madhalimu hawastahiki kabisa kuwa katika sehemu ya uimamu na kuwa mahali pa uongozi), [Kashful asrar, 107-108].

(Kakika chimbuko la amali za Omar ni ukafiri na uzandiki na kwenda kinyume na aya ambazo zimetajwa katika Qur-an), [Kashful asrar, 116].

19. Alkhomeiny anasema: Hakika waislamu huko akhera hawatopata fadhila na rehema za Allah, hizo ni kwa ajili ya Shia tu peke yao!

Amenukuu Alkhomeiny hadithi kutoka kwa Swaduuq: (Hao ndio Allah anaobadilisha mabaya yao kuwa mema, na Allah ni msamehevu na mwenye kurehemu), kasema (as): "Ataletwa muumin mwenye madhambi siku ya kiyama atasimamishwa uwanja wa hisabu, Allah atakuwa ndie mwenye kumuhisabu, hakuta kuwa na mtu yeyote atakaejua, atamtambulisha madhambi yake, atakapokiri makosa yake Allah huwaambia waandishi: Yabadilisheni yawe ni mema na yatokezeni kwa watu, hapo watu watasema: Mja huyu hakuwa na kosa hata moja! Kisha Allah ataamuru apelekwe peponi, hii ndio tafsiri ya aya, na hii ni kwa wenye madhambi katika mashia wetu tu". Alkhomeiny kaitolea maelezo riwaya hii akasema:

(Inajuilikana kwamba jambo hili ni lashia wa Ahlul bayt tu, watu wengine haliwahusu. Kwa sababu imani haipatikani isipokua kwa njia ya wilaya wa Aliy na mawasii wake watoharifu walioepushwa na madhambi (as), bali imani ya kumuamini Allah na Mjumbe wake haikubaliwi bila ya kuamini wilaya kama tutakavyotaja hayo katika mlango unaofuata), [Al arbauna haditha, 511].

20. Alkhomeiny anasema: Watu wa Irani ni bora kuliko watu wa Hijaz katika zama za Mtume (saw)!!

(Mimi nina dai kwa kujiamini kwamba watu wa Irani kwa mamilioni yao zama hizi za sasa ni bora kuliko watu wa Hijaz katika zama za Mtume (saw), na ni bora kuliko watu wa Kuufa huko Iraq katika zama za Amiril Muuminin na Al Husain ibni Aliy (as). Watu wa Iraq na wa Kuufa walifanya muamla mbaya sana na Amiril Muuminin na wakamuasi, na malalamiko ya Imam dhidi yao yanajuilikana katika vitabu vya historia na tarekh, na waislamu wa Iraq na wa Kuufa wamefanya waliyoyafanya kwa Sayyid Shuhadaa (Alhusain ibnu Aliy), hao ni wale wasiotenda dhambi ya kumuua, wakawa ima wamekimbia vita au wamekaa mpaka yakatokea mauaji hayo ya kihistoria). [Al waswiyyah assiyasiyya al ilahiyya lil Imam Alkhomeiny, 27].

21. Alkhomeiny ametoa fatwa ya kuhalalisha mali ya sunni na kwamba haijuzu kumsalia na kwamba sunni ni najisi!

(Ndio, itakuwa si unyanganyi, kutoka kwa muislamu au dhimmiy au mwenye ahadi na mfano wao miongoni mwa watu wanao heshimiwa mali zao. Na kauli yenye nguvu ni kumuunganisha sunni na watu wa vita katika kuhalalisha ngawira kutoka kwao na kwamba mali hizo zina stahikiwa na khumus, bali dhahiri ni kujuzu kuchukua mali zao popote zitakapoonekana na kwa hali yoyote), [Tahrir al wasila 1/251].

(Wala haijuzu kumsalia kafiri wa aina mbali mbali hata murtadi na pia yule aliye hukumiwa ukafiri miongoni mwa wanaojinasibisha na uislamu kama vile masunni na makhawarij), [Tahrirul wasila, 1/80].

(Masunni na Khawarij Allah awalaani ni najis bila ya shaka yeyote), [Tahrirul wasila, 1/118].

22. Alkhomeiny anasema: Kuweka mkono wa kulia juu ya mkono wa kushoto inabatilisha sala isipokua kama ni kwa Taqiyyah!!

(Na la pili, yaani katika mambo yenye kubatilisha sala, ni ukafiri, nako ni kule kuweka mkono mmoja juu ya mwengine kama inavyofanywa na watu wengine, na hilo lina batilisha sala akifanya kwa makusudi, sio kwa kusahau, pamoja na kwamba vizuri zaidi ni kusali tena, lakini itafaa katika hali ya Taqiyya), [Tahrirul wasila, 166].

PILI: SIASA ZA ALKHOMEINY

Baadhi ya waislamu wa mashariki na magharibi walifurahi na kutarajia kheri wakati Mapinduzi ya Irani yalipo fanikiwa, mwishoni mwa miaka ya sabiini katika karne iliyopita. Walidhania kuwa ni ushindi wa uislam na waislamu, na kwamba ni nukta ya kuanzia katika kuikomboa Palestina kutoka katika mikono ya Wazayuni, kwa kauli mbiu zinazo tajwa na viongozi, wakiongozwa na Alkhomeiny. Na ni kweli kwamba kauli mbiu hizo zilikua zina mvuto sana, zinavuta hisia za waislamu kwa vile walijua kwamba haya ni Mapinduzi ya waislamu wanao dhalilishwa duniani na shetani mkuu Marekani, na kwamba yataunga mkono kadhia adilifu, ikiwemo kadhia ya Palestina ambayo waliahidi kuikomboa kutoka katika mikono ya Mayahudi.

Lakini mwenendo wa Alkhomeiny na siasa zake zilionyesha kwamba kauli mbiu hizo zilikua ni jambo la kuwavuta waislamu na kuwapumbaza tu, na lengo lake kuu lilikua ni kutanua Mapinduzi hadi katika nchi za Kiarabu na Kiislamu na kuzitawala tawala zake ili ziwe ni wafuasi wa Mtawala Faqihi.

Alkhomeiny alilitangaza kwa uazi katika sherehe za kwanza za kumbukumbu ya Mapinduzi 11/2/1980 pale aliposema: "Sisi tunafanya utanuzi wa Mapinduzi yetu kwenda katika sehemu nyengine za ulimwengu".

Na katika athari za kutanua Mapinduzi, Alkhomeiny aliwahamasisha Walinzi wa Taifa wa Kiirani kuuwa mahujaji, mnamo siku ya mwezi 6 mfunguo tatu mwaka 1407. Ilitokea fitna kubwa ambayo ilitetemesha ulimwengu, na mbabe na mchochezi wake alikuwa ni Ruhullah Alkhomeiny mwanadini na ibada ambae alishikilia msimamo wa kukoleza fitna hii pamoja na tahadhari na maombi mbali mbali yaliyotolewa.

Ulimwengu uliwashuhudia Walinzi wa Taifa wa Kiirani ambao walijificha kwa kuvaa nguo za mahujaji, wakihalalisha ardhi tukufu na kusababisha fitna ambayo iliacha mamia ya wafu na maelfu ya majeruhi. Fitna hiyo ilianza kwa maandamano yaliyo onekana kwa sura ya nje kuwa ni ya amani, kisha yakabadilika. Waandamanaji wakawa wamebeba visu, vitu vyenye ncha kali na petrol, huku wakinyanyua picha ya Alkhomeny mchochezi na mkolezaji wa fitna hii.

Na kuhusu muelekeo huu wa khatari wa Alkhomeiny dhidi ya nchi za Kiarabu na Kiislamu anasema Mussa Almuusawy: "... Alkhomeiny alikamata utawala ghafla bila ya matarajio ya mtu yeyote, hata yeye

mwenyewe alikua halitarajii jambo hili wala haliwazi, na kwa ajili hiyo haikua mbali kwa mfano wake kufikiria kutanua Mapinduzi ya Irani ambayo aliyaita'', Mapinduzi ya Kiislamu kwenda nje ya mipaka ya Irani. Kwa vile Mapinduzi ya Irani yamefanikiwa kwa namna ambayo hakuifikiria yeye wala mwengine, kwanini yasiweze kufanikiwa katika nchi jirani za Kiarabu ambazo kwa mujibu wa mawazo yake ni shamba lililo tayari kuotesha fikra zake?, hasa ukizingatia kwamba ni lazima kuwa wameathirika na Mapinduzi ambayo matokeo yake ni kuanguka kwa dola kuu jirani kwa muda mfupi. Na kama mbavyo kubahatika kwa kushtukiza kulileta mafanikio kwa Mapinduzi ya Irani, hivyo hivyo kujirejea kwa hali kama hiyo katika nchi jirani ambazo watu wake walifurahishwa na Iran katika siku zake za mwanzo ni jambo linawezekana.

Chuki za ndani alizokua nazo Alkhomeiny zikaanza kufanya kazi, akaichagua Iraq kuwa ni kituo cha mwanzo cha kutanua Mapinduzi, lakini wakati huohuo hakuacha kuzifikiria nchi nyengine jirani. Vyombo vyake vya khabari vililenga mashambulizi makali dhidi ya nchi za Ghuba na kuwatishia adhabu kali, na kuwaonya viongozi wake kuwa yatawakumba yaliyo mkumba Shaah na wasidizi wake. Na hivi ndivyo namna Alkhomeiny alivyovunja mawasiliano baina yake na majirani zake, tokea mwanzo wa kukamata utawala, akatupilia mbali mawazo mazuri ya akili njema, ujirani mwema na maslahi ya Irani, tabia za uislamu na muongozo wa Qur-an isemayo: ''Shikamaneni na kamba ya Allah nyote wala msitengane, na kumbukeni neema ya Allah juu yenu pale mlipokuwa maadui akaunganisha baina ya nyoyo zenu mkawa kwa neema zake ni ndugu, na mlikua karibu na shimo la moto akakuokoeni, hivi ndivyo Allah anavyokubainishieni aya zake ili mpate kuokoka''.

Kuhusu falsafa ya Alkhomeiny ya kutanua Mapinduzi yake na utawawala wake katika eneo hilo, anasema Tarita Barzy : ''....Mwanasiasa mmoja wa Kiirani ambae yuko katika kambi ya wanamageuzi anaielezea Falsafa ya Kiirani kwa namna ifuatayo: '' Fikiria kama utakua na uwezo wa kumuangusha Saddam Hussein na kusimamisha Dola ya Kiislam huko Iraq (.... Kutawala eneo lote kwa ufupi). Utakua na Jamhuri ya Kiislam huko Iraq na Jamhuri ya Kiislam ya Iran, na hizo ndizo nchi mbili zenye nguvu katika eneo hilo. Jambo hilo litapelekea kubadilika kwa mezani ya kila kitu na utakuwa na uwezo wa kuitawala mashariki ya kati yote.

Maneno haya yanaelezea siasa halisi anayoifuata Alkhomeiny na kundi lake la Kiswafawiyya, na mkakati wake wa kutaka kuzipindua Serikali za nchi jirani, na kusimisha serikali za kishia ambazo zitamfuata yeye. Na ikawa Iraq ndio mlengwa wa mwanzo kwa sababu ndio nchi pekee ya kiarabu yenye nguvu kubwa za kijeshi katika eneo hili,kwa hiyvo kuitawala Iraq maana yake ni kutawala eneo lote.

Na waafuasi wa Alkhomeiny walifata mwenendo huo huo lakini kwa njia tofauti na namna mbali mbali, na bado hawajaacha uchokozi wa wazi kama ilivyokua zamani. Wamepanga mpango wa muda mrefu ambao utatimiza utanuzi wa mpango wao wa kibaguzi katika nchi za Kiarabu na Kiislam, na kutimiza ndoto yao ya kiutawala.

Hii ni kuhusu siasa yake ya mambo ya nje. Ama kuhusu siasa yake ya ndani tunaitaja kwa ufupi kama ifuatavo :

- Kiu ya kutawala na Tamaa ya uongozi : Ni yeye Alkhomeiny ambae alikua akitilia nguvu katika hotuba zake kua yeye hatamani uongozi wala hautaki, bali yeye ni Mlezi wa Mapinduzi tu. Anasema Mussa Al Muusawy: "... Watu wa Irani hawakudhania kwaba kiongozi katika viongozi wa kidini anaweza kupambana kwa ajili ya utawala na uongozi hasa pale ambapo kiongozi huyo mara kwa mara alikua anaelezea kuwa yeye hataki kutawala wala hafikirii kabisa jambo hilo. Kama ambavyo wananchi wa Iranhawa-kufikiria akabisa yakwamba kiongozi wa kidini kama Alkhomeiny anaweza kusema uongo wa wazi mbele ya ulimwengu kisha anapo fikia malengo yake ahadi zote alizo zitoa akazieka chini ya miguu yake."

- Utawa usio na mipaka: pamoja na kwamba wanaharakati mbali mbali na makundi yenye nguvu huko Iran yalishiriki katika kuiangusha serikali ya Shaah, na pamoja na kwamba kila upande ulijiona ndio unostahiki kukamata uongozi wa nchi, lakini wote walikubaliana kumchagua Alkhomeiny kuwa ndie kiongozi wao, na makundi yote kuwa chini ya uongozi wake, kwa kudhania kwamba yeye hapendi uongozi wala hautaki.

- Lakini Alkhomeiny aliwashangaza wote pale alipohodhi madaraka yote ya kuongoza nchi, akawa ni yeye na kundi lake tu, hasa hasa baada ya kupitishwa katiba mpya ya Jamuhuri ya Irani ambayo ilileta nadharia ya utawala wa Faqihi jambo amblo alilizusha Alkhomeiny ili awe na madaraka yasoyo na mipaka, aweze kuyatumia atakavo wakati atakao.

- Amesema Mussa Almusawy: "Hivi ndivyo namna Alkhomeiny alivo ingiza jina lake katika katiba yenye mamlaka ya kuendesha nchi, na akajipa madaraka zaidi ya yale aliyo kuwa nayo Shaah katika katiba ya zamani mara mia moja na moja. Amejipa mamlaka na haki ya kumuuzulu Raisi wa Jamhuri, na kuteua Mawaziri na kuwafuta kazi, na kuteua Mkurugenzi wa mashtaka na Jaji wa Mahkama ya Juu, kama ambavo alijiweka kuwa ndie Amiri jeshi Mkuu wa majeshi."

- Udikteta na kuwafyeka wapinzani: Wananchi wa Iran waliondokana na udikteta wa Shaah na siasa za kiimla zilizo tawala nchi, wakajikuta wameingia katika mikono ya dikteta mwengine ambae hatofautiani na yule wa mwanzo katika kuwatesa na kuwadhalilisha wapinzani. Tofauti pekee baina yao ni kwamba Alkhomeiny alikuwa amevaa joho la Udini lakini Shaah hakuwa hivyo.

- Na hapa tutapambanisha baina ya siasa za Shaah na siasa za Alkhomeiny kama zilivyotajwa na Mussa Almuusawy:

- Alkhomeiny alikuwa akimlaumu Shaah na kumtuhumu kwa kupeleka askari wake kuzima maandamano kwa marungu na risasi za mipira, wakati yeye mwenyewe alimzidi mwenzake katika mas-ala haya, kwani alipeleka askari wake katika mikutano iliyofanywa dhidi yake ili wakazime maisha yao, na vibaraka hao wakati mwingi walikuwa wanatumia silaha za moto kama walivyowafanya mujahidin na wengine pale walipo ua wanafunzi sabiini wa Chuo Kikuu cha Tehran ndani ya eneo la Chuo.

- Alkhomeiny alikuwa anayatetea magazeti ambayo yana mkosoa Shaah

ambayo Shaah alikua ameyaadhibu kwa kuyafungia, wakati yeye alipoingia kwenye serikali alifungia magezeti kadhaa ambayo yalikua yanakosoa siasa zake, bali yeye alikwenda mbali zaidi, kwa kuyataifisha magazeti makuu mfano wa gezeti la Kihan na gazeti la Ittilaaat nakuyafanya ni zumari katika zumari zake.

- Alkhomeiny alikua akiziponda siasa za kiimla za Shaah hasa zile za kuwafyeka wapinzani nje ya nchi kwa kutumia polisi wa siri (saafaak), wakati Alkhomeiny mwenyewe alifuata njia hiyo hiyo pale polisi wake wa siri walipo muua Sayyid Tabaatabaiy huko Washington na kumuua mtoto wa dada yake Shaah aitwae Shahram huko Paris. Kama ambavo polisi wake walifanya majaribio ya mauaji ya dokta Shahbur Bakhtiyar Waziri Mkuu katika zama za Shaah na Banii Sadri Raisi wa mwanzo wa Jamuhuri kipindi hicho na Dokta Ali Amiin Waziri Mkuu wa zamani wa Iran na wengineo.

- Alkhomeiny alikua akizilaani Mahkama za kijeshi ambazo zilikuwa zinatoa hukmu za kifo kwa wapinzani wa serikali ya Shaah, wakati ambapo Mahakama za kimapinduzi za Alkhomeiny ziliwaua mamia ya wapinzani wake ndani ya kipindi cha miaka minne zaidi ya zilivyo fanya Mahkama za Shaah katika kipindi cha miaka thelathini. Na kwa utofauti huo huo watuhumiwa wa kisiasa walikuwa na haki ya kujitetea katika Mahkama za Shaah na pia walikua na haki ya kukata rufaa dhidi ya hukmu zilizo tolewa, wakati katika Mahkama za Kimapinduzi ya Kiislam kulikuwa hakuna utetezi, hakuna rufaa, watu mia moja huuwawa kwa dakika moja.

- Lawama ya msingi katika khutba za Alkhomeiny dhidi ya Shaah ilikuwa ni utesaji uliofanywa na Shaah dhidi ya wachache katika maeneo mbali mbali ya nchi na kutokupewa haki zao za kisheria ambapo Alkhomeiny mwenyewe baada ya kushika utawala aliangamiza makabila mbali mbali mashariki mwa nchi na magharibi yake, makumi ya maelfu yaliteketea, na vita viliendelea baina ya walinzi wa Alkhomeiny na wakurdi, waarabu, wabulushi na waturkuman ndani ya miaka minne ya utawala wake, na hii ni mara mia na zaidi kuliko wale waliouliwa na mtangulizi wake kwa miaka thelathini.

- Huu ni baadhi ya udikteta na maguvu ya Mtawala Faqihi ambaye aliyasifu Mapinduzi yake kwa kuyaita Mapinduzi ya wenye kudhulumiwa na wasiopewa haki!!, na ambayo yameonyesha kwamba Dola yake ni dola ya wanamgambo. (Kwa nyongeza zaidi rejea kwenye mtandao huu : *http://khomainy.com*)

Kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi ni Dola ndani ya dola.

Kikosi cha walinzi wa Mapinduzi - kwa kifursi (baasidran) ni jeshi la kiitikadi na walinzi watiifu wa Mlezi Mkuu wa Jamuhuri ya Kiislamu ya Iran, pamoja na kwamba hawahesabiwi katika mipango ya Taifa kuwa ni sehemu ya nguvu za kijeshi za Iran, lakini walinzi hawa wana uogozi wao unaojitegemea na wanapokea amri zake moja kwa moja kutoka kwa Mlezi Mkuu, na wana madaraka na nguvu kuliko vyombo vyote vya ulinzi.

Nguvu za hali ya juu.

Kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi ya Iran inafikia idadi yao askari 350,000, na hii ni kwa mujibu wa Chuo Cha Kimataifa cha mambo ya Mkakati kilichoko

Londan, lakini Chuo Cha Utafiti wa Mikakati Cha Kimataifa Cha Washington kinaona kuwa idadi ya askari hao haivuki 120,000.

Walinzi hawa wa Kimapinduzi walidhihiri Mei 5 mwaka 1979 baada ya kufanikiwa kwa Mapinduzi ya Kiislamu na kuipindua serikali ya Shaah kwa kupitia amri ya Alkhomeiny kiongozi wa Mapinduzi, na kikawekwa chini ya utawala wa Mlezi Mkuu moja kwa moja. Na lengo kuu la kuanzishwa kwa kikosi hichi ni kukusanya nguvu mbali mbali za kijeshi ambazo zilianzishwa baada ya Mapinduzi katika muundo mmoja utakao tii Serikali na kuihami, na kuweka uiwiyano na jeshi la kawaida ambalo halikushiriki katika Mapinduzi na baadhi ya maofisa wake wakawa bado ni watiifu kwa uongozi wa Shaah.

Na askari wa Basidran wanajuulikana kwa hamasa zao za kidini na utiifu wao mpofu kwa Serikali na utayari wao wa kuitetea dhidi ya adui wa ndani na nje, jambo ambalo limewafanya waheshimiwe na wapewe madaraka makubwa ndani ya vyombo vya Dola katika nyanja zote mbili za kisiasa na kiuchumi.

Na katika mambo yanayoonyesha nguvu kubwa za kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi ndani ya jengo la Dola ni pale mmoja wao kuweza kufikia katika ngazi ya Uraisi wa Jamuhuri, nae ni Raisi wa sasa Mahmuod Ahmadi Najad.

Viungo vya dola

Ahmad Najad baada ya kuchaguliwa ameteua Mawaziri watano kutoka katika Walinzi wa Mapinduzi mbali ya kua makumi ya Wabunge katika Bunge ni askari wazamani wa Walinzi wa Mapinduzi.

Na maofisa mbali mbali wa Walinzi hawa wameingia katika idara nyeti na wengine wakawa ni watendaji wambele katika Idara za Ujenzi na Mafuta.

Na Basidran walikua na mchango mkubwa katika vita dhidi ya Iraq kati ya mwaka 1980 - 1988.

Jeshi hili linaonekana ni jeshi imara ambalo lina miliki silaha aina mbili za anga na baharia ambazo ni maalum kwa ajili yake tu.

Pamoja na kwamba Walinzi wa Mapinduzi wanashirikiana na jeshi katika kutekeleza ulinzi wa mipaka ila silaha zao ni za kisasa zaidi hasa hasa makombora ya shihab3 ya masafa ya mbali.

Kikosi cha Basinj ni miongoni mwa matawi ya Walinzi wa Mapinduzi, na hichi ni mfano wa kikosi cha jeshi, na kimeundwa na vijana na wanafunzi wa vyuo vikuu na inakadiriwa idadi yake kufikia milioni kumi, na wao pia wanafuata amri za Walinzi wa Mapinduzi ambao huwapa mafunzo na kuwapatia silaha.

Uwezo

Walinzi wa Mapinduzi huingia katika miradi mbali mbali ya kiuchumi ambayo inakadiriwa kuwa ni mamilioni ya dola, hasa katika upande wa mafuta na gesi asilia na miundombinu, na huongoza asasi mbali mbali za kifedha kubwa kubwa ndani ya Iran kama vile Idara za uzalishaji na utoaji huduma kama vile Majenzi, Barabara, Mafuta na Mawasiliano.

Walinzi wa Mapinduzi wa Iran wanauwezo mkubwa wa kujihami, mfano mitambo ya makombora yenye uwezo wa kubeba vichwa vya mabomu vina uwezo wa kurembea mabomu 1400 madogo madogo kwenye shabaha. Na baadhi ya maofisa wanaeleza kuwa katika walinzi hawa kuna maelfu ya askari waliopewa mafunzo ya kutekeleza mashambulizi ya kujitoa muhanga.

Walinzi wa Mapinduzi wa Iran wameboresha nguvu zao za kijeshi katika miaka ya hivi karibuni kwa namna ya kushtusha, mbali ya mazoezi ya kivita wanayofanya katika vipindi mbali mbali vya mwaka. Na viongozi wa chombo hichi wameboresha silaha mbali mbali hasa katika suala la utengenezaji wa ndege zisizo na rubani na makombora ya shihab 1,2,3 pamoja na mifumo ya ulinzi wa anga na vita vya electcron.

Wakati ambapo makombora ya Shihab3 yanafikia masafa takriban ya 300km, wataalamu wa Kiiran wameboresha makombora ya shihab4 na shihab5 na inategemewa kufikia umbali wa 5000km.

Na katika mtiririko wa vita baridi, Basidran wanakuwa na maonyesho ya silaha mpya za kisasa kila baada ya muda, na hufanya majaribio ya silaha nyengine na kusema kwamba zimevumbuliwa au kuboreshwa na wataalamu wa Kiirani.

Na suali hapa ni: Vipi ndani ya Dola inayojiheshimu kunakua na kikundi kinacho miliki nguvu kama hizi kisha kikawa hakiko chini ya Serikali wala hakiwezi kushtakiwa?

Iran na utanuzi wa Mapinduzi

Utanuzi wa Mapinduzi ni moja ya misingi muhimu ya Mapindunzi aliyoyanadi Alkhomeiny wakati alipo kamata utawala. Ametumia kila alichoweza na kukusanya kila aina ya msaada kutoka kwa wafuasi wake na watu wanaomuunga mkono.

Je ni Misingi gani alitaka kuyatoa nje ya nchi? Na ni njia gani ambazo alitumia?

Alkhomeiny alitangaza katika moja ya hotuba zake tarehe 11/2/1980: "Hakika sisi tutatanua Mapinduzi yetu kwa ulimwengu wote mpaka kila mmoja ajue kwa nini tumefanya Mapinduzi "

Maana ya kutanua Mapinduzi

Baada ya Mapinduzi ya Alkhomeiny dhidi ya Shaah mwaka 1979, kwa miezi kadhaa Iran iliboresha mahusiano yake na baadhi ya nchi za Kiarabu ikiwemo Siria, Lebanon, Aljazair, Vyama vya Kipalestina na Libya, na utawala wa Kimapinduzi huko Iran ukategemea kuwa na mahusiano mazuri na nchi za eneo hilo, kwa kutumia fursa ya tangazo la Shaah wa Iran la kujenga mahusiano na Israil,na ghadhabu za waislam zilizojitokeza wakati huo baada ya tangazo hilo, na Dola mpya ya Kiiran ikawa inafanya jitihada ya kujiondoshea tuhuma ya ubaguzi ambayo mara nyingi ilikua inasifikana nayo.

Lakini hali hii ilipokosekana kwa sababu mbali mabli nzito ikiwemo vita baina yake na Iraqi, Iran ilijikuta katika hali tete, na kwamba Dola la Kimapinduzi ni lenye kuelekezewa uadui, hivyo ni lazima kupata marafiki, washirika na waungaji mkono kwa ajili ya kujihami na kupata utulivu **, na hapo ndipo Iran ikaanza kujitafutia makundi badala ya nchi.**

Na hapa ndipo ilipozaliwa falsafa ya "Kutanua Mapinduzi", na nadharia hii imeitumikia na kuisaidia Iran sana, lakini wakati huo huo imeisababishia madhara makubwa, kwani imeipa mahusiano makubwa na mazito na makundi mbali mbali, lakini kwa upande mwengine ikaikimbiza na kuiweka mbali na nchi nyingi.

JARIBIO LA KUTANUA MAPINDUZI KWENDA KWENYE MAENEO MENGINE:

Kuanza kwa vita vya Iraq na Iran ni matokeo ya siasa hiyo, ambapo

wahanga wake walikua ni zaidi ya watu milioni moja na laki tano, vita vilianza mwaka 1980 na kuendelea mpaka mwaka 1988. Msingi wa kutanua Mapinduzi ambalo ni tangazo lililotolewa na Alkhomeiny ilikua ni moja ya sababu kuu ya vita hivi.

Hali hiyo iliambatana na kujiingiza kwa Iran nchini Lebanon na jaribio la kuanzisha Dola ya kishia kupitia Harakat al-amal na baadae Hizbullah, waliowapa mafunzo na kuunda kikosi cha wanamgambo wenye silaha ndani ya Lebanon, silaha ambazo zilikuwa ni juu zaidi ya jeshi la serikali.

Ndani ya Yemen, Iran ilianzisha wanamgambo wa Kihuthi na kuwajengea uwezo wa kimali na kisilaha na kupewa mafunzo ndani ya Iran na kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi, kwa lengo la kuandaa kikosi kitakachoweza kusababibisha vurugu. Wahuthi walianza kujaribu kuharibu usalama wa Saudia kwa kueneza fitina za kimakundi kusini ya Saudia na wakati mwengine kwa mashambulizi ndani ya Saudia ambayo yalizimwa na jeshi la Saudia. Baaad ya kushindwa mara kadhaa likaanza kupambana na jeshi la Yemen na kuwashughulisha na kutoa ulinzi wa nchi na kulipoteza nguvu zao, na kusababisha vifo vya Wayemen wengi hadi kufikia kuweza kuutwaa mji wa Sanaa na ndipo pakaanza ukombozi wa Yemen ujulikano kwa (Kimbunga cha uhakika).

Nchini Iraq, baada ya kuangushwa serikali ya Baath, Iraq iligeuka kuwa ni upande wa pili wa Teheran na kuwatawalisha waungaji mkono wake, kuanzisha makundi mbali mbali ya wanamgambo wenye silaha mfano wa Ahli al-haq, Faylaq al-badri, na zaidi ya makundi ishirini yenye silaha, yote yalijiingiza kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe na kueneza mifarakano baina ya suuni na shia wa Iraq, miripuko ikasambaa kila sehemu, mauji ya kikabila na migomo ya kimakundi, kitu ambacho kilipelekea miji ya Iraq kuwa ni vijiji vyenye silaha, wakakosa maisha ya ushirikiano yaliyokuwapo kabla baina ya Wairaq, na wahanga wa mapambano haya wakazidi milioni moja, mauji ambayo hawakusalimika watoto, wanawake, wala wazee.

Na nchini Saudia tunakumbuka matokeo ya milipuko ya kigaidi iliyotokea katika moja ya msimu wa hija, tukio ambalo wahanga wake walikuwa zaidi ya mahujaji elfu tano, kwenye njia ya chini kwa chini ya Almuaysim, na watu zaidi ya elfu kumi wakajeruhiwa. Na wahalifu walikiri kuwa walimwaga kemikali za sumu, jambo lililosababisha kuumia na kufa watu wengi waliokuja kwa ajli ya ibada ya hija.

Na katika mwaka 1989, kulitokea mauaji ambayo mikono ya Wairani haikuwa mbali nayo kwenye msikiti mtukufu wa Makka

Syria pia hali ni ile ile, Iran ilijiingiza tangu mwanzo wa machafuko, na ikaunga mkono utawala wa Asaad baada ya kuona nchi za kiarabu imeupa mgongo, na kutangaza kumuunga mkono kwa hoja ya kuzuia na kupambana na uzayuni katika eneo hilo, na kuhahikiksha kuwa pamoja nae kwa ushindi au kufa nae, na Qasim Suleimany kiongozi wa faylaq alquds na mmoja wa viongozi wa Walinzi wa Mapinduzi ya Iran ndie kiongozi halisi na ndie anaeongoza mapambano ya Asad huko Syria.

Na huko Bahrein kwa kupitia mchezo wa kuigiza wa -Dawaar luluat- Iran imesaidia waasi na kujaribu kutaka kuipundua, na wakati huo huo inavikalia kwa mabavu visiwa vitatu vya Tawala za Kiarabu ambavo ni (Tumbul kubra, Tumbu sughura na Abuu Mussa), na inakataa aina yoyote

ya mazungumzo au hata kutafuta ufumbuzi katika mahakama za kimataifa.

Kuweit nayo kamwe haikusalimika na njama za Kiiran, na kiongozi wake Marehemu Sheikh Jabir Alsabah alikumbana na jaribio lililoshindwa la kumuuwa kupitia mpiganaji wa kujitoa muhanga wa kundi la Hizbu daawa la Iraq, linaloungwa mkono na Iran. Kuweit iliituhumu rasmi Iran kuwa nyuma ya jaribio hilo, nayo ni kwa sababu ya msimamo wa Kuweit wa kuunga mkono Iraq katika vita vyake na Iraq.

Na bila ya kusahau Ahawaz ya Kiarabu iliyoiteka Iran kwa makubaliano na Uingereza mnamo April 25/1922, nayo ilikuwa ni Dola ya Kiarabu yenye kujulikana na maendeleo yake ni zaidi ya miaka elfu saba, na pamoja na hayo ulifutwa utambulisho wake wa Kiarabu kikamilifu, hali ya kua wakazi wake ni wa makabila ya Kiarabu halisi.

Mchezo kama huu umefanyika kwa njia nyengine kwa kutaka kupeleka nadharia ya Mapinduzi ya Kiirani ndani ya Misri, kupitia majaribio mbali mbali ya kufungua mlango wa utalii wa kidini kwa baadhi ya maeneo yanayotukuzwa ndani ya Misri, kwa lengo la kuingiza fikra na utamaduni wao.

Na matukio yamethibitisha kwamba, makusudio ya kutanua Mapinduzi ni kuwaamsha wafuasi wa kishia popote walipo nje ya Iran, na kuwahamasisha wasijichanganye na watu wa eneo lao, na wajitenge kijamii na kitamaduni. Na kwa upande mwengine kuwaunganisha kisiasa na kiuchumi na Walii Faqihi huko makao makuu pamoja na kuhakikisha kwamba hawatengani moja kwa moja na watu wa maeneo yao bali waungane nao kwa hali ya kujilinda na kuweza kuathiri muda wote jamii na nchi wanazoishi, chini ya mwevuli wa uananchi au haki za wachache au jenginelo. Na kwa ibara nyengine yaendelee kubaki makundi haya ya kishia kama viungo vya mbali ambavo Tehran itavitumia kwa malengo yake ndani ya kila jamii na nchi waliko bila ya kutumia nguvu za moja kwa moja ambazo zinagharama wala hazina ulazima.

Dola la Wanamgambo na Kudhulumiwa kwa Ahli Sunna huko Iran

Mtafiti Swabbaah Al Musawiy ameelezea kudhulumiwa kwa Ahli Sunnah kwenye makala yake, anasema: ''Ni jambo lisilo shaka kwamba dhulma na mateso yameenea kila sehemu huko Iran chini ya Wilaayatul Faqiih, lakini viwango vya dhulma hizo na mateso hayo hutofautiana baina ya kundi moja na jengine.

Kwa mfano dhulma inayomfika mfaris na shia kwa ujumla haiwezi kulinganishwa na dhulma anayoipata ahli Sunnah na asiyekuwa mfurs. Ahil Sunna ambao wengi wao ni wakurdi, Mabalushi, Warabu na Waturkamana, hao hufikwa na dhulma na unyanyasaji mchanganyiko wa kikabila na kimadhehebu.

Na mateso ya Ahlul Sunnah huanza kwa mas-ala madogo madogo kwendea kwenye makubwa zaidi, na mateso haya baadhi yake ni matokeo ya kanuni na katiba, na mengine hutokana na matendo ya wafanyakazi wenye ubaguzi kwenye vyombo vya dola. Mateso haya yamejikita kwenye maeneo matano; ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kidini.

Kwenye Uwanja wa kisiasa:

Huangaliwa Ahli sunnah kwamba wao ni upande usio kuwa rafiki na usiokuwa na haki yoyote ile na huonekana kuwa ni wananchi wa daraja la pili, na dalili ni kwamba Katiba ya Irani inashurutisha kuwa Rais wa Jamhuri lazima awe ni shia wa madhehebu ya Kiithnaashariyyah na

kiutekelezaji wadhifa huu utakua umeondoshwa toka kwa Ahli Sunnah huku jina la dola ni Jamhuri ya Kiislamu ya Irani (kama wanavyodai), na mustalahi wa Jamuhuri unamaanisha uongozi ni wa kiraia ambao unamaanisha haki sawa kwa wote. mustalahi wa Kiislamu unamaanisha muislamu mwenye kufata Dini ya Kiislamu, na katika anwani na tafsiri hizi hazikuashiria cho chote kile kuhusiana na usunni na ushia. Na hapa inabainika kwamba kuna ufahamu mwengine kwa viongozi wa utawala wa Kiirani, hasa hasa kwamba wao daima wanazungumzia kuhusiana na utawala wa kiraia wa Kiislamu na sio uongozi wa kimakundi ya kiraia.

Kunyimwa kwa Ahli Sunna kushika madaraka hakukuishia kwenye cheo cha mshauri wa Raisi wa Jamhuri au Waziri au Msaidizi wa Waziri, lakini umefikia mpaka kwenye uongozi wa kata, au kiongozi wa kijeshi au polisi, kama vile ambavyo Wizara ya Usalama au ile ya Mambo ya Nje haina mfanyakazi wa kisunni hata mmoja mwenye cheo japo cha chini kabisa, na iwapo watakuwepo wafanyakazi wadogo wadogo kwenye Wizara ya Mambo ya Nje (nao wapo kwenye kukaribia kustaafu) basi hao ni mabaki ya wafanyakazi walioajiriwa zama za utawala uliopita.

Ubaguzi huu mwingi wao unatokana na sharia na matoleo yasiyoandikwa yanayohusiana na kuamiliana na Ahli Sunna. Na hii inapingana na kipengele cha cha (19) cha katiba ambacho kinasma: Kwamba Wairani kutoka asili yoyote au kabila au madhehebu yoyote, wako na haki sawa, lakini pamoja na kupita miongo mitatu ya uongozi wa Jamhuri ya Irani kipengele hichi na na mfano wake bado havija tekelezwa.

Uwanja wa kiuchumi:

Maeneo ya mipakani mwa Irani Mashariki, Magharibi, Kaskazini na Kusini ni katika jamii sizizokuwa za Kifursi na wengi wao ni katika Ahli Sunnah, na maeneo haya ndiyo maeneo mafukara zaidi, na pamoja kauli mbiu ya kuwatetea wanyonge ambayo hurudiwa rudiwa na viongozi wa Irani kila wakati, ila kamwe hawajachukua hatua yoyote ile ya uhakika kuhusiana na ujenzi wa maeneo haya ili kuipa ukweli kauli mbiu yao tuliyoitaja hapo kabla, kwani bajeti yote ya serikali iliyowekwa kwa ajili ya matumizi ya maeneo ya Ahli Sunnah katika kipindi chote cha miongo mitatu-maiaka thelathini -iliyopita hailingani na bajeti ya eneo moja tu katika maeneo makuu yasiyokuwa ya Ahli Sunnah.

KWENYE ENEO LA KIJAMII:

Katika mambo yanayosikitisha ni kwamba sheria zinazotumika na hatua za kibaguzi zinazofanywa, zimekuwa na athari mbaya kabisa, na siku hadi siku ufa baina ya Wafursi na jamii nyengine kwa upande mmoja na baina ya Ahli Sunnah na Shia kwa upande mwengine umekua ukiongezeka, kama ambavo juhudi za kuwaweka mbali na Serikali wasiokuwa Wafursi na Ahli Sunnah zinazidi kupamba moto zaidi na zaidi.

Kama vile ambavyo hatua ya uenezaji wa madawa ya kulevya kwenye maeneo ya Ahli Sunnah mashariki, magharibi na kusini mwa nchi, ambayo yalionakana hapo kabla kua ni maeneo yenye kulinda heshma, yamegeuka sasa na kua ni maeneo yaliyoharibika kabisa na kuzama kwenye utumiaji wa madawa ya kulevya, hali ambayo inaleta mashaka hata kwenye hisia za watu wa kawaida na kupata masuali ya kujiuliza, ni nani anaesimama

nyuma ya uingizaji na uenezaji wa madawa ya kulevya kwenye maeneo yao?, vipi vyombo vya usalama viweze kufichua na kukitia nguvuni haraka kikundi kidogo cha kisiasa kinachofanya shughuli zake kwa siri katika maeneo haya ya Ahli Sunnah, lakini waonyeshe kutokua na uwezo na wanshindwe kuchukua hatua za haraka dhidi ya wasambazaji wa madawa ya kulevya ndani ya maeneo haya?.

KWENYE ENEO LA UTAMADUNI:

Kama tulivyotangulia kusema kwamba Ahli Sunnah wengi wanapatikana kwenye jamii zisizo za kifursi, na wengi wao ni kutoka kwenye jamii za Kikurdi, Balushi, Waarabu na Waturkuman, na jamii hizi zina tamaduni zake, lakini zinanyimwa kupata haki zao za kitamaduni. Kipengele nam.(15) cha katiba kinatowa haki ya mtu kusoma kwa lugha yake maskulini, sambamba na lugha ya kifursi lakini bado kipengele hicho hakijatekelezwa.

Kwenye eneo la kidini:

Pamoja na kuwepo kipengele nam (12) cha katiba ya Iran ambacho kimewapa wafuasi wa madhehebu mbali mbali ya Kiislamu (Hanafy, Shaafiy, Maaliky, Hambaly, na Zaydy) uhuru wa kutekeleza mipango yao kwenye mas-ala ya usomeshaji, malezi ya kidini, mambo ya kijamii (Ndoa,Talaka, Mirathi na Wasia) na yanayohusiana na madai kwenye mahkama, lakini hilo bado halijaizuwia serikali kuingilia mambo ya kidini ya Sunni, kwa mfano kufungwa kwa maskuli ya kidini yanaotambulika na kuteua maimamu wa sala za jamaa na kuwaondoa baadhi ya viongozi wa kidini mashuhuri wenye kuheshimika na wenye hadhi kubwa kwenye jamii ya kisunni na kudogosha umuhimu wa mashekhe wa kisunni na kuwadhalilisha kwa kuwapa mishahara duni na kuwaweka foleni kwa ajili ya kuwalipa mishahara yao, kuingilia kati njia na mihutasari ya ufundishaji kwenye madrasa zao za kidini za asili na zenye mizizi kwenye utamaduni wa madhehebu ya Ahli Sunnah, na kuanzisha madrasa mpya za kidini zinazofanya kazi chini ya usimamizi wa Wizara ya Usalama. Uingiliaji kati huu umeibua hasira na hali ya kutoridhika kwa Ahli Sunnah na hasa hasa maulamaa wao. Na cha kuzingatia zaidi ni kwamba markazi kubwa ya Kiislamu iliyoanzishwa kwa ajili ya usimamizi na ufatilaji wa mambo ya Ahli Sunnah, pamoja na kuwepo mashekhe wakubwa miongoni mwa Ahli Sunnah ila viongozi na waendeshaji wote wa markazi hii ni watu wa Dini wa kishia tu.

Pamoja na hayo yote pia kuna upungufu wa vituo vya utamaduni kwenye maeneo ya kisunni wakati serikali bado inazidi kuendelea kujenga vituo vya Huseiniyyaat na vituo vya utamaduni wa kishia kwenye maeneo yenye masunni wengi na kinyume chake wanazuwia miskiti ya Kisunni kwenye maeneo yenye mashia wengi, kwa mfano Utawala unazuwia ujenzi wa msikiti wa kisunni Tehran mji wenye idadi ya Sunni milioni moja na nusu na hivyo hivyo Asfahan, Ahwaz na kwengineko.

Mambo ya nje ya saudia: Hizi ni dalili za msaada wa Iran kwa ugaidi ulimwenguni. [1]

Inawezekana ikawa Tangazo la Wizara ya Mambo ya Nje ya Saudia ndio taarifa bora zaidi iliyoelezea muhtasari wa maovu ya Dola ya Wanamgambo

[1] http/www/Al Arabiyyah

wa Kikhomeiny, kwani Taarifa hii imeyataja maovu hayo yote na kuyaratibu kwa mujibu wa terahe yalipofanyika, na kubainisha kuwa historia ya Iran tokea Mapinduzi yake ya mwaka 1979 imejaa kampeni za kueneza fitna, vitisho na machafuko katika nchi za eneo hili, kwa lengo la kudhoofisha usalama na amani ya nchi hizi huku ikipuuza sheria, mikataba, makubaliano ya kimataifa na misingi ya tabia njema. Saudia kwa kipindi chote hicho imekuwa ikivumilia, pamoja na shida na mitikisiko inayoipata yeye, nchi za eneo hili na ulimwengu kwa ujumla unaotokana na siasa za kiuadui za Kiirani.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Saudia imetayarisha ripoti yenye idadi na tarehe za matukio, na inaweka wazi siasa za kiuadui za Irani kwa kipindi cha miaka 35, na kuzima madai ya uongo ya Utawala wa Tehran wa kujitakasa.

Na ufuatao ni uchambuzi wa rikodi ya Utawala wa Iran katika kusaidia ugaidi na uasi kwenye eneo hili na Ulimwenguni kwa ujumla.

1- Irani ndio nchi ya mwanzo duniani kulea na kudhamini ugaidi. Imeanzisha taasisi kadhaa za kigaidi ndani ya nchi (failaqul Quds na njenginezo), na nje ya nchi, Hizbullah Lebanon, Hizbullah Hijaaz, wanamgambo wa Ahlil Haqq Iraq, na wengi wengineo, pamoja na makundi mbali mbali ya wanamgambo wa kikabila kwenye nchi mbali mabli, wakiwemo Wahuthi wa Yemen, ambapo Umoja wa Mataifa umeitia hatiani na kuiwekea vikwazo.

2- Mwaka 1982 kulifanyika utekaji nyara wa raia (96) wa kigeni huko Lebanon wakiwemo wamarekani 25, kwa kile kinachojuilikana kuwa ni mzozo wa mateka ambao uliendelea kwa muda wa miaka kumi, sehemu kubwa ya shughuli za utekaji nyara zilitekelezwa na Hizbullah, na makundi yanayofadhiliwa na Iran.

3- Mwaka 1983 ulipuwaji wa ubalozi wa Marekani huko Beirut uliofanywa na Hizbullah chini ya ufadhili wa Utawala wa Iran, na kusababisha kuuawa watu 63 kwenye ubalozihuo.

4- Mnamo mwaka 1983 mtu mwenye uraia wa Iran 'Ismail Askary ' ambae ni askari wa kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi, alitekeleza shambulio la kujitowa muhanga huko Beirut lililotayarishwa na Iran kwenye kambi ya askari wa miguu wa Kikosi cha Baharia cha Marekani na kuuwa watu (241) na kujeruhi zaidi ya watu (100) askari wa kikosi hicho cha Bahariya na raia wa kimarekani. Magazeti ya Marekani yameitaja idadi hii ya wahanga kuwa ndio kubwa zaidi kuwahi kutokea nje ya uwanja wa mapambano.

5- Mwaka 1983 kulifanyika ulipuaji kwenye kituo cha Kifaranza huko Beirut uliotekelezwa na Hizbullah, sambamba na ulipuaji wa kituo cha kimarekani uliouwa wafaransa 63 kati ya raia na askari.

6- Mwaka 1983 wanamgambo wa Hizbullah na Hizbu Daawa wanaofadhiliwa na Iran kilitekeleza mashambulizi kadhaa kwenye ubalozi wa Marekani na Ubalozi wa Ufaransa huko Kuweit, vile vile mashambulizi hayo yalilenga pia kituo cha kusafishia mafuta na baadhi ya mitaa na yaliwauwa watu wa tano na kujeruhi wengine nane.

7- Mnamo mwaka 1983 meli za mafuta za Kuwait zilishambuliwa katika eneo la Ghuba na kulazimika kupeperusha bendera ya Marekani.

8- Mwaka 1984 Hizbullah walitekeleza shambulizi dhidi ya mwambata

wa kibalozi wa kimarekani huko Beirut Mashariki, na kusababisha kuuwawa watu 24 wakiwemo wamarekani.

9- Mwaka 1985 jaribio la kulipua msafara wa Amiri wa Kuweit Marehamu Sheikh Jaabiril Ahmad As Swabaah uliopelekea kuuawa kwa maaskari na kujeruhi raia kadhaa wa Ghuba.

10- Mwaka 1985 Utawala wa Iran ulitekeleza utekaji nyara wa ndege ya Shirika la ndege la (TWA) na kuwazuwia abiria 39 wa kimarekani kwa muda wa wiki kadha na kuua askari mmoja wa kikosi cha Baharia cha Marekani aliekuemo kwenye ndege hiyo.

11- Mwaka 1986 Iran iliwachochea mahujaji wake kufanya vurugu kwenye msimu wa Hijja, jambo ambalo lililopelekea msongamano na kufariki mahujaji 300.

12- Mnamo mwaka 1987 warsha ya kituo cha mafuta cha Ras Tanurah Mashariki ya Saudia ilichomwa moto na wafuasi wa kundi la Hizbullah Hijaaz linaloungwa mkono na Iran, na mwaka huo huo kikundi cha Hizbullah Hijaaz kilishambulia shirika la Swadaf kwenye mji wa viwanda wa Jubail Mashariki mwa Saudia.

13- Mwaka 1987 Utawala wa Iran ulitekeleza mauwaji ya mwanadiplomasia wa Saudia Musaid Al Ghaamidy, Allah amrehemu huko Tehran, na ni mwaka huo huo liliozimwa jaribio ya Iran la kuingiza vilipuzi Saudia kupititia mahujaji wake.

14- Mnamo mwaka 1992 Utawala wa Iran ulilipua mkahawa Mikonos huko Barlin ambapo mwanasheria mkuu wa Shirikisho la Ujerumani alitowa hati ya kukamatwa Waziri wa upelezi wa Irani Aliy Falaahayyaan kwa tuhuma za kupanga na kusimamia ulipuaji wa mkahawa huo na kuwauwa wakurdi wanne wapinzani waliokuwemo ndani ya mkahawa huo wakati wa mlipuko.

15- Mwaka 1994, Iran ilifanya ulipuaji huko Boines Ires na kuuwa zaidi ya watu 85, na kujeruhi wengine 300. Na mnamo mwaka 2003 Polisi wa Uingereza walimkamata Hadi Bour Balozi wa zamani wa Iran nchini Argentina, kwa tuhuma za kufanya njama za kutekeleza mashambulizi.

16- Mnamo mwaka 1996 wana mgambo wa Hizbullah Hijaaz inayoungwa mkono na Utawala wa Iran walilipua makaazi ya watu huko Khubar na kuuwa watu 120 kati yao (19) ni raia wa Marekani. Iran ilitoa hifadhi kwa watekelezaji wa shambulio hilo, akiwemo raia wa Saudia Ahmad Al Mughasal ambae alikamatwa mwaka 2015 akiwa na uraia wa Iran. Shambulio hili la kigaidi liliongozwa na aliekuwa mwambata wa kijeshi wa Kiirani nchini Bahrein wakati huo, ambapo watekelezaji wa shambulizi hili walipata mafunzo nchini Iran na Lebanon na uingizaji wa vilipuzi kwenda Saudia ulifanywa na Hizbulla. Serikali ya Saudia na serikali za mataifa rafiki wana ushahidi wa kutosha juu ya matukio hayo.

17- Mnamo mwaka 2003 mpango wa Kiirani wa kutekeleza mashambulizi ya kigaidi huko Bahrein ulifanikiwa kuzimwa, baada ya kutiwa nguvuni kikundi kipya cha kigaidi ambacho kinafadhiliwa na kikosi cha walinzi wa Mapinduzi cha Iran pamoja na Hizbullah ya Lebanon, na majaribio kama haya yamefanywa pia Kuweit na Falme za Kiarabu kwa nyakati tofauti.

18- Mwaka 2011 Utawala wa Iran ulitekeleza mauwaji ya mwanadiplomasia wa Saudia Hasan Al Qahtwaany, Allah amrehemu huko Karachi.

19- Mnamo mwaka 2011 Marekani ilizima jaribio la kuuwawa kwa Balozi wa Saudia na ikathibitika kwamba Utawala wa Iran ulikua nyuma ya jaribio hilo, ambapo Mahkama ya Muungano ya New York ilitaja majina ya watu wawili waliopanga jaribio hilo katika kesi ya jinai iliyofunguliwa Mahakamani hapo, nao ni Mansour Arbaabisyaar, ambae alikamatwa na kuhukumiwa kifungo jela miaka 25, na mwengine ni Ghulam Shukry ambaye ni ofisa kwenye kikosi cha walinzi wa Mapindunduzi cha Iran aliyepo Iran, na ambae Mahakama ya Marekani bado inaendelea kumtafuta.

20- Mwaka 2016 Mahkama ya jinai ya Kuweit ilitowa hukumu ya kifo dhidi ya watu wiwili waliopatikana na hatia kwenye kesi maarufu ijuilikanayo kwa **khaliyyatul Ibadly** (kikundi cha Ibadly) mmoja wao ni raia wa Iran, na walishtakiwa kwa makosa ya kutenda matendo ambayo yanapelekea kuvunjika kwa amani na mshikamano wa Taifa la Kuwait na kufanya ujasusi pamoja na Iran na Hizbullah kwa lengo la kufanya matendo ya kiuadui.

21- Mnamo mwezi wa January mwaka 2016 Iran ilikiri rasmi kupitia kamanda wa kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi cha Iran Muhammad Ali Jaafary kuwepo kwa wapiganaji 200,000 wa Kiirani nje ya nchi yao huko (Syria, Iraq, Afaghanistan, Pakistan na Yemen).

22- Vile vile Maofisa wa kibalozi wa Kiiran waliunda mitandao mbali mbali ya kijasusi katika mataifa mbali mbali ili kutekeleza mashambulizi ya kigaidi kupitia vikundi hivyo. Na katika nchi ambazo ziligundua kuwepo kwa mitandao hiyo ya kijasusi ya Kiirani kwenye ardhi zao ni pamoja na : Saudia mwaka 2013, Kuweit miaka ya 2010, 2015, Bahrein miaka ya 2010, 2011, Kenya mwaka 2015, Misri miaka ya 2005,2008, 2011, Jordan mwaka 2015, Yemen mwaka 2012, Imaraat mwaka 2013,Turkey mwaka 2012 na Nigeria mwaka 2015.

23- Mbali na Hizbullahi ya Lebanon, ambayo Naibu Waziri wa mambo ya nje wa Marekani Richard Armitag ameitaja kuwa ni taasisi ya mwanzo ya kigaidi duniani, utawala wa Iran umeanzisha vyama na vikosi vya wanamgambo mbali mabli vya kigaidi huko Iraq, Yemen na kwengineko ambayvo inavitumia kwa kuharibu amani na kuondosha utulivu.

24- Vile vile kuingiza askari wa kikosi cha Walinzi wa Mapindunduzi huko Iraq ili kutoa mafunzo kwa wanamgambo wa kishia, na kuwatumia katika kuwauwa vijana wa kisunni na majeshi ya Kimataifa.

25- Utawala wa Iran ndilo taifa lenye kusambaza zaidi dunuani milipuko ya (**IED**), ambavyo hutumika katika kulipulia magari na vifaru**,** na imesababisha kuuwawa kwa mamia ya wanajeshi wa Kimataifa huko Iraq.

26- Utawala wa Iran ndio wa mwanzo kushambulia ofisi za kibalozi kuanzia uvamizi wake dhidi ya Ubalozi wa Marekani mwaka 1979 na kuwateka maafiasa wake, kwa muda wa siku 444, na kufuatiwa na uvamizi dhidi ya Ubalozi wa Saudia mwaka 1987, uvamizi dhidi ya Ubalozi wa Kuwait mwaka 1987, uvamizi dhidi ya Ubalozi wa Urusi mwaka 1988, mashambulizi dhidi ya mwanadiplomasia wa Kuwait mwaka 2007, uvamizi dhidi ya Ubalozi wa Pakistan mwaka 2009, uvamizi dhidi ya Ubalozi wa Uingereza mwaka 2011, na mwisho uvamizi dhidi ya Ubalozi

wa Saudia na Conseli yake huko Mash-had mwaka 2016.

27- Eneo la Bara Arabu kamwe halikuwahi kujuwa ukabila wala umadhehebu ila baada ya kufanyika Mapinduzi ya Iran mwaka 1979. Utawala wa Iran uliingilia nchi za Lebanon, Syria,Iraq na Yemen, mpaka mmoja wa wasaidizi wake ambae ni Haidar Muslihy Waziri wa zamani wa upelelezi wa Irani akasema kwa kiburi kabisa kwamba Iran inatawalia miji mikuu mine ya Kiarabu.

28- Mfano mkubwa wa Iran wa kuingilia mambo ya nchi za eneo hili ni kuingia kwake kwa kishindo huko Syria na kupeleka askari wa kikosi chake cha Walinzi wa Mapinduzi na Failaq Al Quds, na kuunda kikundi cha wanamgambo cha Hizbullah, na wanamgambo wa kikabila kwanye nchi kadhaa, na kumsaidia Bashaaril Asad katika vita dhidi ya raia wake ambavyo vimepelekea mauaji ya zaidi ya raia 250,000 wa Syria na kuzalisha wakimbizi karibu milioni kumi na mbili, maafa ambayo hayajawahi kutokea katika historia ya hivi karibuni.

29- Uingiliaji huu wa Irani katika mambo ya ndani ya nchi za eneo la Bara Arabu, hakukupingwa na Saudi Arabia peke yake, bali pia umepingwa na Umoja wa nchi za Kiarabu kwa nguvu zote kwenye maazimio yake yote, likiwemo azimio lake la hivi karibuni katika Kikao cha dharura cha Baraza la Mawaziri kwenye mkutano wake wa mwisho siku ya jumapili tarehe 10/1/2016.

30- Utawala wa Iran unatiwa hatiani na jamii ya Kimataifa na Umoja wa Mataifa kwa kuvunja haki za binadamu, na kufadhili ugaidi jambo ambalo linasisitizwa na azimio nam.411/70 la Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa lililotolewa tarehe 6/10/2015.

31- Kulingana na ripoti za Kimataifa, hukumu za vifo nchini Iran zimepindukia elfu moja katika kipindi cha mwaka 2015, yaani kwa kiwango cha watu watatu kwa siku moja, na kiwango hichi cha hukumu za kifo kilipanda katika miezi saba ya mwanzo ya mwaka 2015. Mahakama ya juu imetia saini hukumu za kifo 27 dhidi ya maulamaa wa Ahli Sunnah, bila ya sababu yoyote ile inayopelekea mafano wa hukumu hizo.

32- Iran inavunja haki za wachache zikiwemo zile za makabila ya Kiarabu, Kikurdi, Balushi na wengineo, ambayo hunyimwa kupata haki zao.

Mwisho wa ripoti ya Wizara ya Mambo ya nje ya Saudia.

Na baadaya maelezo hayo yenye ushahidi, jee kuna mwenye akili anaetilia shaka kuwa Dola hii haifuati Sharia za Kiislamu wala sheria za Kimataifa ? Na kwamba sheria na kanuni zake ni vikosi vya wanamgambo wa kigaidi?

Mwisho:

Baada ya hayo imeshabainika wazi kwamba Alhomeiny ndiye dira ya Dola ya wanamgambo, na yeye ndie marejeo. Amejenga dola isiyoheshimu sheria na isiyo na uadilifu kwa asiyekuwa shia, na kwa kutumia anuani ya kutanua Mapinduzi ameeneza ufisadi kwenye nchi za Kiislamu za Kisunni, kusababisha fitna na kuchochea chuki, na mrathi wake Al khaaminiiy amefuata nyayo zake kikamilifu.